



# CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII UFUNDI MISUNGWI

S.L.P 2799 MWANZA| Barua pepe: [pmissungwi@jamii.com](mailto:pmissungwi@jamii.com) Tovuti: [www.misungwicdtti.ac.tz](http://www.misungwicdtti.ac.tz)

---

---

## TAARIFA KWA UMMA

### KUCHAGULIWA KWA WANAFUNZI NA OFISI YA RAIS TAMISEMI KUJIUNGA NA PROGRAMU YA UHANDISI UJENZI NA MAENDELEO YA JAMII (CIVIL ENGINEERING WITH COMMUNITY DEVELOPMENT- NTA LEVEL 4) MWAKA WA MASOMO 2024/2025

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi (Misungwi Community Development Technical Training Institute) ni Chuo cha Serikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kipo wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza na kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa nambari **REG/EOS/015** na kupata ithibati kamili (Full Accreditation).

Chuo kinapenda kuwapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kwa mafunzo mwaka wa masomo 2024/2025 kwa fani ya Uhandisi Ujenzi na maendeleo ya jamii kwa ngazi ya NTA Level 4. Chuo kitaendelea kushirikiana na NACTVET na OR TAMISEMI katika kutoa taarifa sahihi kwa wote waliochaguliwa ikiwa ni pamoja na kuweka maelekezo ya kujiunga na chuo (Joining Instructions) kwa ajili ya wazazi/walezi na wataanzania wote kupata taarifa zote na mahitaji kwa mwanafunzi.

Mambo ya kuzingatia kwa wataanzania

1. Chuo kinawasisitiza waliochaguliwa wote kuepuka utapeli kwa watu wasiowaaminifu
2. Kuwasiliana na Chuo mara kwa mara wakati wote wa maandalizi
3. Maelekezo ya Kujiunga na chuo yanapatikana kupitia tovuti ya chuo [www.misungwicdtti.ac.tz](http://www.misungwicdtti.ac.tz)
- 4.

Chuo kinawakaribisha wote waliochaguliwa kujiunga na programu ambayo wamechaguliwa kwa kuwa ina tija kwa Taifa katika kupunguza changamoto ya mafundi sanifu Ujenzi (Civil Engineering Technicians) kwa maendeleo endelevu ya Taifa..

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi |+255713197574|+255653118018|+255672566076

IMETOLEWA NA:  
CHARLES F. ACHUODHO  
MKUU WA CHUO  
TAREHE: 30 MEI 2024

*Misungwi CDTTI - The Home of Engineers*